



NIT YATOA MAFUNZO YA USALAMA BARABARANI MKOANI DODOMA



Na Juma Manday

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeshiriki katika maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani (Road Safety Week 2024) ambayo yameratibiwa na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani yenye kaulimbiu “Endesha Salama Ufike Salama”. Maadhimisho hayo kitaifa yamefanyika Mkoani Dodoma katika Uwanja wa Jamhuri kuanzia tarehe 26 hadi 31 Agosti, 2024 ambapo yalifunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango tarehe 26 Agosti, 2024 na kufungwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile tarehe 30 Agosti, 2024.

Katika maadhimisho ya mwaka 2024, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kupitia kituo chake cha Umahiri cha Kikanda katika Usalama Barabarani (RECoERS) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kitengo cha Elimu ya Usalama Barabarani kimetoa elimu ya usalama barabarani kwa makundi mbalimbali mkoani Dodoma ikiwemo madereva bodaboda, wanafunzi wa shule za msingi, na madereva wanaosomea udereva wa awali.

Kwa upande wa wanafunzi wa shule za msingi, Chuo kimetoa mafunzo ya usalama barabarani kwa wanafunzi wa shule za msingi kumi na moja (11) Mkoani Dodoma. Mafunzo hayo yamefanyika wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani tarehe 28.08.2024 na 29.08.2024 yakihusisha shule za msingi za Mazengo, Kikuyu, Uhuru, Amani, Mlezi, Mlimani, Makole, Kizota, Chadulu, Mlimwa na Kisasa.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkoani Dodoma Mkuu wa Kituo cha Umahiri cha Kikanda katika Usalama Barabarani - NIT Ndg. Godlisten Msumanje amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea wanafunzi wa shule za msingi uelewa wa matumizi sahihi ya barabara.

“Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea wanafunzi hawa uelewa wa matumizi sahihi ya barabara ikiwemo sehemu salama za kuvuka barabara, aina za vivuko vya barabara, maeneo hatarishi kuvuka barabara, kanuni ya kuvuka barabara nk”.

Pia Ndg. Msumanje aliongeza kuwa Chuo kupitia kituo chake cha Umahiri cha Kikanda katika Usalama Barabarani kimetoa mafunzo ya usalama barabarani kwa madereva wanaosomea mafunzo ya awali. Mafunzo hayo yamefanyika tarehe 29.08.2024 Mkoani Dodoma wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani kwa madereva wanaosomea mafunzo ya awali – VETA Dodoma.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea wanafunzi hao uwezo katika masuala ya usalama barabarani ikiwemo ukaguzi wa magari, udereva wa kujihami, sheria na kanuni za usalama barabarani, alama na michoro barabarani nk.

Vilevile Chuo kimetoa mafunzo ya udereva wa magari ya mizigo (HGV) kwa madereva Mkoani Dodoma. Mafunzo hayo ya siku kumi na tatu (13) yamefanyika wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani kuanzia tarehe 19.08.2024 hadi 31.08.2024 ambapo jumla ya madereva kumi na nne (14) walihudhuria mafunzo hayo na kutunukiwa vyeti.

Akizungumza na washiriki wakati wa hafla ya kufunga mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Idara ya TSEE, Bi. Lydia Kamugisha amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo na umahiri madereva hao katika kuendesha magari ya mizigo kwa kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani.

Katika maadhimisho ya kitaifa ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani 2024 wadau mbalimbali wa masuala ya usalama barabarani walishiriki ikiwemo NIT, LATRA, Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Wizara ya Uchukuzi, Jeshi la Polisi Kitengo cha Elimu ya Usalama Barabarani, TANROADS, NMB, CRDB, VETA, ATC.

MATUKIO KATIKA PICHA



Wakufunzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) wakiwa na washiriki wa mafunzo ya udereva wa magari ya mizigo (HGV).



Wakufunzi kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) wakiwa pamoja na baadhi ya wanafunzi wanaosomea mafunzo ya awali ya udereva - VETA